

Nyimbo:Pesa

Mwimbaji: Remmy Ongala

Video URL: <http://www.youtube.com/watch?v=0gAQyUFNNXE>

Maana ya maneno (words and Expressions explained)

Mafanikio – success

Unipe (kupa) – to give

Niwe (kuwa) – to be

Matumizi – expenditure

Walimwengu – people

Utafika (kufika) – to arrive

Manoti – money

Hela/pesa – money

Shauri ya – because of

Wandugu (ndugu) – relatives

Watakufata (kufuata) – to follow

Ukikosa (kukosa) – to miss

Kudharau – to despise

Wakazi – residents

Usione aibu (kuona aibu) – to feel shy

Maswali (Questions)

1. Nyimbo hii inahusu nini?
2. Mwimbaji anasema nini kuhusu umuhimu wa pesa? Taja matatu ambayo ukiwa na pesa unaweza kuyapata.
3. Nini matokeo ya kukosa pesa kwa wakazi wa Dar es salaam?
4. Mwimbaji anazungumzia kazi mbalimbali ambazo unaweza kufanya ili upate pesa. Taja kazi tatu.
5. Nyimbo hii ina ujumbe gani kwa jamii?

Mazoezi (exercises)

1. Sikiliza nyimbo halafu jaza mapengo

Nalia pesa, _____ pesa, niwe kama wewe

Nalia pesa, pesa ni _____ kwa matumizi ya walimwengu,
popote utapokwenda bila pesa hakuna _____

Ukiwa na pesa _____ utapotaka utafika

Ukitaka pesa _____ manoti atakushauri, manoti pesa, manoti ee, manoti hela,
manoti ooo

Pesa baba yako ni nani? Pesa _____ walimwengu tungelikuuliza kwa nini
wengine wanao na wengine wao hawana

Halafu unajiuliza kwanini _____ yako ana nyumba, na mimi sina nyumba, shauri ya
pesa

_____ na pesa wandugu watakufata eee, ukikosa pesa _____

Jamani pesa, nalia pesa eee, unipe pesa,

Sisi _____ wa Dares salaam hatuna shamba ooooo, shamba letu ni pesa,
ukikosa pesa unalala _____, ukikosa pesa unadharaulika,

Ukitaka kutafuta pesa usione _____, ukiuza _____ utapata pesa, ukiuza
_____ utapata pesa, ukiuza _____ utapata pesa, ukiuza
_____ utapata pesa,

haya yote _____ kuyapata bila kufanya kazi kwa _____

Na pia huwezi kuyapata haya yote bila kuzingatia _____, Yashinda pesa, Ali pesa,
Hamisi pesa,

Kanyole pesa, nalia pesa oo, unipe pesa, manoti pesa, manoti pesa, pesa ooooooooo

2. Andika kwa ufupi nyimbo hii inazungumzia nini.

3. Unafikiri mtu anaweza kuishi bila ya kufanya kazi? Kwanini?

4. Andika sentensi zenye maana kwa kutumia maneno yafuatayo:

- i. Kudharau
- ii. Matumizi
- iii. Kuona aibu
- iv. Njaa
- v. Wakazi